BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Nane – Tarehe 19 Mei, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

51. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa miongoni mwa majukumu ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni kutoa mitaji na kusaidia kutafuta masoko kwa wajasiriamali. Na kwa kuwa Jeshi letu la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) linatekeleza jukumu la kuwafunza vijana kuhusiana na kujiajiri kwa kufanya ujasiriamali. Na kwa kuwa kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuunganisha uratibu wa taasisi hizi mbili ili tija ipatikane, mathalan, baada ya vijana kumaliza mafunzo ya JKU kupatiwa vifaa na maeneo ya kufanyia kazi.

(a) Je, Serikali inaionaje hoja hii.

(b) Je, tathmini ya Serikali ikoje katika kutekeleza suala hili.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

104. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na wimbi linaloongezeka la magari ya ng'ombe yanayoendeshwa wakati wa usiku bila ya taa wala 'reflectors' katika maeneo ya Zanzibar hasa hasa katika barabara ya Fuoni–Kombeni, jambo ambalo husababisha ajali za kutisha. Kinachosikitisha zaidi ni kwamba hakuonekani kuwepo juhudi rasmi zinazochukuliwa na Serikali katika kukomesha jambo hili.

(a) Je, ni kesi ngapi zimeripotiwa katika mwaka 2021-2022 za magari ya ng'ombe yanayoendeshwa wakati wa usiku bila ya taa wala 'reflectors'.

(b) Je, ni ajali ngapi zimeripotiwa katika mwaka 2021-2022 zilizosababishwa na magari ya ng'ombe yanayoendeshwa wakati wa usiku bila ya taa wala 'reflectors'.

(c) Je, ni zipi juhudi na kauli ya Serikali katika kudhibiti magari ya ng'ombe yanayoendeshwa wakati wa usiku bila ya taa wala 'reflectors'.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

32. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Wizara tayari imeshaanza kujenga uzio katika Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Vitongoji, na kwa kuwa uzio huo umefikia karibu ya asilimia 60 ya ujenzi wake na bado asilimia 40 ili kukamilika kwake.

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa uzio huo ili kukiweka chuo hicho katika hali ya utulivu na amani kwa wanafunzi pamoja na walimu wao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

21. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali imeanza utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji nchini. Hata hivyo, kumekuwa na mapungufu katika kuandaa makadirio ya mahitaji ya maji kulingana na muda wa mradi huo.

Je, ni kwa namna gani changamoto hii imezingatiwa katika miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa.

**Wizara ya Afya:**

102. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Utaratibu mpya umewekwa na Serikali wa kuangalia wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja mara mbili kwa siku, yaani saa 12 asubuhi na saa 10 jioni tu. Utaratibu huu unaleta usumbufu kwa baadhi ya wananchi hasa wanaotoka mbali na Mkoa wa Mjini Magharibi na Dar es Salaam ambao wana nia ya kurudi siku hiyo hiyo baada ya kumuona mgonjwa, kwa sababu utaratibu huu haukuzingatia ufikaji na uondokaji wa vyombo kutoka na kufika Zanzibar na Dar es Salaam.

(a) Je, ni ipi mantiki halisi ya kuwa na utaratibu huo mpya wa kuangalia wagonjwa.

(b) Je, kwa kiasi gani utaratibu huo mpya umeleta ufanisi wa kutibu ukilinganisha na ule utaratibu wa zamani wa mara tatu kwa siku (asubuhi, mchana na jioni).

(c) Je, Serikali haioni haja na ulazima wa kuwapa utaratibu bora wenye kutoa tahfifu kwa wananchi wanaotoka mbali na Mkoa wa Mjini Magharibi na Dar es Salaam wenye wagonjwa wao Hospitali na wanaotaka kurudi siku hiyo hiyo baada ya kumuona mgonjwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

85. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaishukuru Serikali kwa kutoa fursa kwa vijana wetu hapa Zanzibar kujiajiri kupitia usafiri wa boda boda. Hata hivyo, tokea kuruhusiwa kwa usafiri huu, tumeshuhudia vifo vingi na ulemavu mbali mbali kutokana na ajali zinazokithiri nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha darasa la elimu ya barabarani na matumizi mazuri ya vyombo ili kupunguza vifo na ulemavu unaotokea.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
19 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA